# TIMER NATIONAL SERIES
# MAJARIBIO YA MTIHANI {6}
## DARASA LA SITA KISWAHILI

CODE0072021

Muda: Saa 1 Dak 40

**Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya uliyopewa.**

__1__ kutoka shuleni __2__, Kajembe aliiwasha __3__ ili kupata __4__ ya kukitazama kipindi alichokipenda __5__ dhati. Alipokuwa shuleni mchana huo, mwalimu __6__ wa Kiswahili aliwaagiza __7__ matangazo yaliyohusu madhara __8__ __9__.

1. A.Baada B. Baada ya C. Kabla ya D. Kabla
2. A. jioni hiyo B. usiku huo C. siku hii D. jioni hii
3. A. redio B. panka C. runinga D. rununu
4. A. nafsi B. fuska C. fursa D. wasaa
5. A. kwa B. katika C. kwenye D. ndani ya
6. A. wake B. wao C. huyu D. ule
7. A. wakayatazame B. wayatazame C. wakaione D. wazione
8. A. ya B. za C. wa D. la
9. A. madawa ya kulevya B. dawa za kulevya C. mihadarati za kulewesha D. mihadarati

__10__ yanayohusiana na ajira za watoto __11__ __12__ na kila mwanajamii aliye timamu. Kwa hakika, kumwajiri mtoto __13__ unyama tu bali pia ni ukosefu wa maadili. Ni jukumu la kila __14__ wetu kuukataa unyama huu. Tukishirikiana kupinga kwa pamoja tutafaulu kwani __15__.

10. A. Maswala B. Masuala C. Matatizo D. Matangazo
11. A. wamekuwa B. zimekuwa C. imekuwa D. yamekuwa
12. A. zikipingwa B. ikipingwa C. yakipingwa D. wakipingwa
13. A. ni B. ndiyo C. ndiye D. si
14. A. mmoja B. moja C. umoja D. pamoja
15. A. kawia ufike
    B. kidole kimoja hakivunji chawa
    C. mwenda tezi na omo marejeo ni ngamani
    D. akili nyingi huondoa maarifa

***Kutoka swali la 16 hadi 30, jibu swali kulingana na maagizo.***

16. Ni gani kati ya vyombo hivi hakipatikani sebuleni?
A. Picha
B. Shubaka
C. Rafu
D. Godoro

17. Tumia kivumishi cha pekee **–o-ote** kujazia pengo.
Zifueni nguo
A. zote
B. yoyote
C. zozote
D. yote

18. Jibu maamkizi yafuatayo.
Je, mhali gani?
A. Nzuri
B. Vyema
C. Ni salama
D. Tu wazuri

19. Ni sentensi gani haijatumia kivumishi cha sifa?
A. Mwaka huu utaisha lini?
B. Watu wawili wamefika.
C. Mtoto mdogo ameanguka.
D. Tunda hili ni bichi.

20. Huyu ni jasiri kuliko wengine wote.
Neno lililopigiwa mstari ni mfano wa
A. kiashiria
B. kiwakilishi
C. kivumishi
D. nomino

21. Gani kati ya mavazi haya ni mfano wa kofia?
A. Tarbushi  B. Joho
C. Surupwenye  D. Jezi

22. Tumia kiulizi **–ngapi** kwa ustadi.
Ni nyuzi ____ zilizokatika?
A. mingapi  B. ngapi
C. vingapi  D. mangapi

23. Chagua sentensi iliyotumia **–amba** kwa usahihi.
A. Ugonjwa ambayo unatisha ni huo.
B. Mikanda ambazo zinavutia ni hizi.
C. Wao ndio ambayo walitumwa.
D. Ambao hawana vitabu waje.

24. Ni sentensi gani imetumia lugha ya adabu?
A. Dada yake alizaa pacha.
B. Chopoo ni mwizi sana.
C. Bwana Kapombe amevaa miwani.
D. Mgonjwa amehara tena.

25. Kiambishi ki cha udogo kiko katika sentensi gani?
A. Kibuzi changu hakitachinjwa.
B. Kioo changu kimevunjika.
C. Chandarua kimefuliwa tena.
D. Kiswahili ni lugha nzuri.

26. Andika idadi ifuatayo kwa maneno.
Vikombe 13 ndivyo vipya.
A. Kumi na tatu
B. Vikumi na tatu
C. Kumi na vitatu
D. Vikumi na vitatu

27. Kanusha kauli ifuatayo.
Wewe umeimba vizuri.
A. Wewe haujaimba vizuri.
B. Wewe hujaimba vibaya.
C. Wewe hujaimba vizuri.
D. Wewe haujaimba vibaya.

28. Nimeula uyoga wangu.
Tambua wingi wa sentensi hii.
A. Nimeula uyoga wenu.
B. Tumeula yoga zetu.
C. Nimeula yoga zao.
D. Tumeula uyoga wetu.

29. Chagua majina yaliyo katika ngeli moja.
A. Maji, maumbo
B. Magonjwa, manukato
C. Marashi, maisha
D. Mazingira, maiti

30. Mimi na sisi, wewe na nyinyi, yeye na wao ni mifano ya
A. vielezi
B. nafsi
C. vivumishi
D. nomino

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 hadi 40.***

Likizo iliyopita ilijawa na shughuli nyingi kupita kiasi. Pindi tu shule zilipofungwa, nilipata nafasi kumzuru bibi mzaa baba katika kijiji cha Jipindeni. Sikuenda Jipindeni peke yangu. Nilikuwa na mama na dada yangu, Jerusha. Baba alibaki mjini Angaza tulipokuwa tukisoma. Naye hakubaki peke yake bali alibaki na kaka yetu aliyekuwa wa kwanza katika familia yetu, Omieri.

Haja yangu kubwa zaidi kumzuru bibi ilikuwa ni kujifunza mengi kuhusiana na mambo ya shambani na kazi ya ukulima kwa jumla. Nilifanya hivyo kwa sababu ndoto yangu ukubwani ilikuwa kuwa mkulima hodari wa kusifika.

Kwanza nilijifunza kunyunyizia mimea maji katika msimu wa kiangazi ambazo huwa kuna jua kali bila mvua. Maadamu tulifika kijijini katika msimu huo, hatukuwa na budi kuenda mtoni kila asubuhi na jioni kuteka maji ili kuinyunyizia mimea michanga, yaani miche. Hili tulifanya na bibi tu.

Si hayo pekee, nilijifunza kutayarisha shamba huku nikiongozwa kufyeka nyasi na magugu kwa kutumia <u>kwanja</u>. Hakika, nilifurahia sana kazi hiyo. Ilipoisha, bibi alituongoza na Jerusha hadi katika josho ambapo tulimsaidia bibi kuwaelekeza mifugo humo jashoni ili wakaoshwe na kuondolewa wadudu kama vile kupe.

Siku zilipozidi kusonga, tulijifunza kuchunga huko milimani. Ingawa kazi hii ilichosha kwa ajili ya usumbufu wa baadhi ya wanyama hasa mbuzi, nilikuwa na fahari kwani sikuwa nimewahi kuchunga. Zaidi ya hayo, nilifurahia jinsi ambavyo baadhi ya mifugo wetu walinitegea masikio nilipowaita kwa majina.

**31.** Kulingana na aya ya kwanza, shule zilipofungwa mwandishi alimtembelea nani?
A. Mke wake
B. Rafiki yake
C. Wazazi wake
D. Nyanya yake

**32.** Mwandishi alijifunza haya yote wapi?
A. Angaza B. Jerusha
C. Omieri D. Jipindeni

**33.** Familia ya mwandishi iliyoishi mjini ilikuwa na jumla ya watu wangapi?
A. Watano
B. Wanne
C. Sita
D. Watatu

**34.** Badala ya kutumia neno **"kwanja"** mwandishi angetumia neno gani?
A. Fyekeo B. Sururu
C. Msumeno D. Shoka

**35.** Haja kubwa zaidi ya msimulizi kumzuru bibi ilikuwa gani?
A. Kumjulia hali.
B. Kuwachunga mifugo.
C. Kujifunza mengi ya ukulima.
D. Kutayarisha shamba.

**36.** Kina Jerusha walifika kijijini katika majira gani?
A. Kiangazi B. Masika
C. Vuli D. Kipupwe

**37.** Kulingana na ufahamu mifugo huoshewa wapi?
A. Mtoni B. Mlimani
C. Joshoni D. Malishoni

**38.** Kati ya wanyama hawa ni gani hawakuwa wakichungwa mlimani?
A. Mbuzi B. Ng'ombe
C. Swara D. Kondoo

**39.** Kulingana na mwandishi wanyama gani waliokuwa wasumbufu zaidi?
A. Wote B. Mbuzi
C. Ng'ombe D. Kondoo

**40.** Kulingana na paragrafu ya mwisho
A. baadhi ya wanyama walikuwa na majina.
B. mbuzi walikuwa wasumbufu kuliko wanyama wengine.
C. mwandishi na bibi tu ndio walioenda mtoni.
D. mwanambee wa kina Jerusha alibaki mjini.

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 hadi 50.***

Vijana wengi sana humu nchini hulalamika kuwa hakuna nafasi za kazi nchini. Wengi huonekana wamejikalia katika vikundi vidogo vidogo huku wakihesabu magari yanayopita na kutafunatafuna **maajabu fulani ya kijani**. Jua likisonga, nao wasonga hadi wakati ambapo jua litaaga miti, nao wainuke, wajikukute makalio na kuondoka kuelekea "sijui". Tabia hii inaonyesha uzembe wa hali ya juu. Uvivu huo ukiendelea, vijana hao huenda wasiweze hata kutimiza majukumu rahisi kama kujinadhifisha.

Ukweli ni kuwa, si lazima kazi iwe ni ile ya kuajirwa. Mtu, hasa kijana, anaweza kujiajiri na hata kubuni nafasi za ajira kwa vijana wengineo. Ukulima, kwa mfano ni kazi ambayo vijana wengi sana humu nchini huihusisha na uchafu na kuumiaumia kwingi. Ni vizuri vijana washauriwe kuwa **achanikaye kwenye mpini hafi njaa**. Kazi ya ukulima ni kazi ambayo ina mapato chungu nzima.

Licha ya ukulima, vijana wanaweza kuanzisha vikundi vya kibinafsi kisha baadaye kuomba mikopo serikalini na kuanzisha mipango yao, yaani miradi ya maendeleo kama vile vituo vya uoshaji wa magari, uuzaji wa maua, uuzaji wa vifaa vya ufundi na kadhalika.

Vijana watazidi kuangamia kwa umasikini ikiwa wataendelea kutetewa na wazazi hata baada ya kutimiza umri wa kuoa na kuolewa. Umasikini huo utazidishwa na uigaji duni na uraibu katika mambo ambayo hayana maana. Si hayo tu, **vijana wasiopika wala kupakuwa** wanapokutana katika vikundi vyao wao hupotoshana tu na kwa hivyo, umaskini utazidi miongoni mwao kutokana na shinikizo la hirimu.

---

**41.** Taarifa hii kwa jumla
A. inawashauri vijana.
B. inawakemea vijana.
C. inawasuta vijana.
D. inawagombeza vijana.

**42.** Mwandishi ana maana gani anapotaja "**maajabu fulani ya kijani**"?
A. Gundi  B. Sigara
C. Bazoka  D. Miraa

**43.** Badala ya kutumia neno uzembe mnenaji angetumia neno gani?
A. Mvivu  B. Uvivu
C. Goigoi  D. Bidii

**44.** Mwandishi anasema kuwa ni kazi gani ambayo hudhaniwa kuwa ya uchafu?
A. Uoshaji magari  B. Ukulima
C. Uuzaji maua  D. Uuzaji vifaa

**45.** Ni mradi gani wa maendeleo haukutajwa katika aya ya tatu?
A. Uuzaji wa magari
B. Uoshaji wa magari
C. Uuzaji wa maua
D. Uuzaji wa vifaa vya ufundi

**46.** Kulingana na taarifa, ni gani kati ya haya haitaleta umaskini miongoni mwa vijana?
A. Miigo duni
B. Uraibu duni
C. Kupumzika viwulini
D. Kuishi na wazazi hata ukubwani.

**47.** "**Achanikaye kwenye mpini hafi njaa**" ni
A. nahau
B. tashbihi
C. kitendawili
D. methali

**48.** Vijana "**wasiopika wala kupakuwa**" ni wale ambao
A. hawajui kufanya kazi vizuri.
B. hawajui kupika wala kupakua.
C. wana bidii za mchwa.
D. hawana msaada wowote.

**49.** Mwandishi anasema kuwa vijana wanaweza kuomba mikopo wapi?
A. Kwa wazazi wao.
B. Kwa wenzao wanaofanya kazi.
C. Serikalini.
D. Kazini kwao.

**50.** Kulingana na paragrafu ya mwisho, ni mambo mangapi yanayoweza kuleta umasikini miongoni mwa vijana?
A. Manne
B. Matatu
C. Matano
D. Machache